# PENPLUS TRIAL SERIES

KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

PENPLUS NPS-3

## DARASA LA SABA

## MUHULA WA TATU

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU*** **Muda: Saa 1 Dakika 40**

1. *Tumia penseli ya kawaida.*
2. *Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:*
   *(I) NAMBARI YAKO YA MTIHANI (II) JINA LAKO (II) JINA LA SHULE YAKO*
3. *Kwa kila swali onyesha jibu sahihi kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.*

---

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1-15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

__1__ ya kuidhinishwa kwa __2__ mpya, waliozoea kula vya bure na __3__ mali ya umma wameanza kujipata __4__. Maafisa __5__ wamefikishwa mahakamani au __6__ kufunguliwa __7__. Si ajabu kumpata mmoja wao akidai kuwa __8__ lake linalengwa na kina Muigai.

Wanaopenda kuhepa __9__ mrefu wa sheria wajue kuwa __10__ ki motoni. Mwenzako akinyolewa __11__ tia maji. Elimu __12__ __13__ mkubwa mzazi anaweza kumwachia __14__. Nasi wana tunapaswa __15__ ili tufaidike masomoni.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. badala | B. kati ya | C. kabla | D. baada |
| 2. | A. ratiba | B. serikali | C. katiba | D. rais |
| 3. | A. kuvuja | B. kufuja | C. kuvunja | D. kufunja |
| 4. | A. mashakani | B. mastaka | C. mashtaka | D. mlango |
| 5. | A. wafisadi | B. wema | C. wakorofi | D. wachanga |
| 6. | A. shuleni | B. kortini | C. hospitalini | D. kotini |
| 7. | A. washtaka | B. mastaka | C. mashtaka | D. mashitaka |
| 8. | A. watoto | B. nyumba | C. familia | D. kabila |
| 9. | A. moto | B. mguu | C. mkono | D. mtu |
| 10. | A. chama | B. chadalua chao | C. chumba chao | D. chuma chao |
| 11. | A. chako | B. chenu | C. chetu | D. chao |
| 12. | A. ndiyo | B. ndio | C. ndivyo | D. ndicho |
| 13. | A. uriidhi | B. uriithi | C. uridhi | D. uridi |
| 14. | A. mwanao | B. mwanake | C. mwanawe | D. mwanaye |
| 15. | A. kutoa bidii | B. kutia bidii | C. kuweka budi | D. kufanya budi |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30 chagua jibu lililo sahihi.***

16. Ng'ombe ni kwa zizi, ________ ni kwa ndege.
A. nyumba
B. kiota
C. mti
D. utando

17. Nyama hushikiliwa na nyama zinazoitwa ________
A. shavuu
B. shavu
C. koo
D. ufizi

18. Chagua sentensi ambayo ni sanifu.
A. Mali yake yote yaliibiwa.
B. mtake huyo wote utaliwa
C. Gari ile ni ya kaka.
D. Chungwa lake limeliwa

Andika kinyume cha:-

19. Saibu amemfuta kapera.
A. Ajuza amemwajiri mwanamwali
B. Ajuza amemfuta kapera
C. Ajuza amemwajiri mwanamwali
D. Ajuza amemfuta mwanamwali

20. Maziwa, mate, machozi na maji yako katika ngeli ya:-
A. YA-YA
B. U-YA
C. I-ZI
D. LI-YA

21. ***Tegua kitendawili***
Afahamu kuchora lakini hajui achoracho ni ________
A. nyoka
B. konokono
C. kobe
D. mjuzi

22. Chagua kiashirishi kisisitizi katika sentensi hii
Mwalimu alitumia kitabu kiki hiki.
A. kiki hiki
B. kitabu
C. mwalimu
D. alitumia

23. Ni kihusishi kipi cha "katika" kinachomaanisha ndani ya?
A. Alienda katika msitu
B. Mto u katika msitu
C. Vitabu vyote vimewekwa katika mfuko huu
D. Kijiko ki katika meza

24. Chagua nomino katika sentensi ifuatayo:-
Aliingia nyumbani na akawasha moto
A. nyumbani
B. na
C. moto
D. akawasha

25. ***Kamilisha methali ifuatayo.***
Haraka haraka haina ________
A. uzembe B. tamaa
C. hasara D. baraka

26. Ndoto mbaya zinastua mtu.
Kisawe cha neno ndoto ni:-
A. ota B. njozi
C. ono D. usingizi

27. Mtu anayewakilisha nchi yake katika nchi ingine huitwa ________
A. balozi
B. mlowezi
C. kibaraka
D. jasusi

28. Ni sentensi ipi iliyo sahihi kisarufi.
A. Embe hii imeoza
B. embe huyu imeoza
C. embe hiyo imeoza
D. embe hili limeoza

29. Mkate ulipoliwa Juma ________ alikuwa.
A. ndiye mwenyewe
B. ndiwe ambaye
C. ndiye ambaye
D. ndiyo ambayo

30. ***Jaza pengo kwa kiwakilishi sahihi.***
Chai tuta ________ pika sisi.
A. ya
B. i
C. ki
D. u

*Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali 31-40.*

Wanafunzi wengi hujikuta katika **udhia** punde tu wapatapo matokeo yao ya mtihani wa mwisho wa mwaka. Hii inatokana na kushindwa kuzoa alama walizokuwa wametazamia.

Alama zenyewe hukosekana mara tu mwanafunzi anapoanza kupuuza somo fulani. Kusema kweli, lazima mwanafunzi afaulu katika kila somo kumwezesha kupasi masomoni.

Somo ambalo huwavuja moyo baadhi ya wanafunzi ni somo la uraia na ndini. Wanafunzi wapaswa kuelewa kuwa ndilo somo ambalo hufanya kupasi kuwe nadra iwapo hawatajitolea **udi na uvumba**. Yampasa mwanafunzi awe na nia na **madhumuni** ya somo lolote alisomalo. Isitoshe, mwanafunzi huenda akafeli kwa kutokuwa mwadilifu.

Somo la Kiswahili hukumbwa sana na tatizo la mwanafunzi kushindwa kusoma na kuelewa. Lakini tatizo kubwa ni ugonjwa wa **uzembe na ugoigoi** wa kutohimiza moyo uwe na tabia na mazoea ya kusoma. Wanafunzi wapaswa kutembelea maktaba za shule zao mara kwa mara.

Katika somo la Kiswahili, wanafunzi wapaswa kuvisoma vitabu vya mashairi vitakavyowawezesha kuamsha uwezo wao wa kufikilia na kwa kufanya hivyo, wataweza kuzoa alama watazamiazo, kwani mtaka cha mvunguni ni sharti ainame.

31. Kulingana na taarifa, wanafunzi wengi hujikuta katika udhia. Nini maana ya udhia?
    A. Nia
    B. Furaha
    C. Usumbufu
    D. Lengo

32. Kwa nini wanafunzi wengi hushindwa na kuzoa alama walizokuwa wametazamia?
    A. Kutia bidii katika baadhi ya somo
    B. Kupuuza baadhi ya somo
    C. Kukosa vitabu katika maktaba
    D. Kupunguka kwa walimu

33. Kitu gani ambacho huwavunja wanafunzi wengi moyo?
    A. Matokeo mema
    B. Udhia
    C. Somo la Kiswahili
    D. Somo la ndini na uraia

34. Mwanafunzi apaswa kujitolea kwa udi na uvumba. Usemi huu unamaanisha nini?
    A. Kujitolea juu chini
    B. Kujitolea vumbini
    C. Kujitoa fumbi
    D. Kujitoa vumbi

35. Kisawe cha neno madhumuni kama lilivyotumika ni:-
    A. Pesa
    B. Lengo
    C. Dohani
    D. Madharau

36. Kulingana na ufahamu, ni tatizo lipi kubwa linalokumba somo la Kiswahili?
    A. Kushindwa na kusoma
    B. Kujitolea kwa udi na uvumba
    C. Ugonjwa wa uzembe na uvumba
    D. Kufeli

37. Kumwezesha mwanafunzi kupasi, apaswa kutembelea:-
    A. wanafunzi
    B. mwalimu
    C. shule
    D. maktaba mara kwa mara

38. Vitabu vya mashairi vina manufaa yapi kwa mwanafunzi kulingana na taarifa?
    A. Huamsha uwezo wa kufikilia
    B. Humsaidia katika utunzi wa nyimbo
    C. Huchekesha
    D. Maswali mengi hutolewa kwenye shairi

39. Methali"Mtaka cha mvunguni sharti ainame" imetumika kaitka taarifa. Taja methali nyingine yenye maana sawa.
    A. Mwenda tezi na omo marejeleo ni ngamani
    B. Haraka haraka haina baraka
    C. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa
    D. Nyoko nyoko ni shibe ya kuonana

40. Kwa ujumla, taarifa hii inatuhimiza:-
    A. Tutilie maanani somo la Kiswahili
    B. Tutie bidii katika kila somo ili tupasi
    C. Umuhimu wa mwanafunzi shuleni
    D. Umunimu wa somo la hisabati

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50.***

Siku ilikucha vibaya kwa mvua, ngurumo na makelele ya umeme. Kwa hali hii, kila mahluki alilazimika kuenda kulala awali ya saa ya kawaida.

Mmuliko mmoja ulipenya nyumbani mwangu, mkawa mweupe kama kwamba na ya umeme. Dakika ile ile nilisikia mnazi ulioko uani ukianguka na mbele barazani kitu kili chunga chunga na kuchacharika. Nilituhumu kwamba kitu hicho kilikuwa kikibari mvua. Dhana zangu ziliniambia kuwa ni nyamaume mawindoni. Basi nilijifunika gubigubi na kulala fofofo.

Asubuhi yake kulikuwa shwali na kutulivu. Nalo jua lilikuwa kali licha ya kuwa saa mbili na nusu nilipo amka. Nilipofungua mlango niliona nyama kubwa imening'inia mlangoni. Pale pale nilifunga mlango kwa hofu na kuduwaa. Nilidhani ni simba kama nilivyokisia jana usiku. Halafu nikafafanua jinsi nilivyomwona tena, nikakumbuka nilimwona akiwa na hatamu na saruji. Nikajua kwamba hakuwa simba ila binadamu.

Nikafungua mlango tena na mnyama huyo akanilaki kwa huzuni. Kisha nikaona macho yake katika mauti. Kwa kuwa nilikuwa karibu na barabara, msafiri huyo alikuwa akitaka kujikinga mvua alipogongwa na radi.

Ama kweli yake ilikuwa bahati mbaya kwa kupata mauti yake.

**41.** Kwa nini watu walienda kulala mapema?

A. Waliogopa mahuluki
B. Kulikuwa na vita nje
C. Waliogopa ya anga iliyotokana na mvua
D. Waliogopa kuvamiwa na majangili

**42.** Mvua, ngurumo na makelele ya umeme yalitokea wakati gani?

A. Wakati wa usiku mchanga
B. Wakati wa asubuhi
C. Wakati wa alfajiri
D. Wakati wa jioni

**43.** Mmuliko uliopenya nyumbani mwa msemaji ulikuwa wa:-

A. taa
B. majambazi
C. askari wa kulinda amani
D. mweso wa umeme

**44.** Ni kitu gani kilichoanguka?

A. Mlango B. Mnazi
C. Mtu D. Simba

**45.** Mnyama aliyekuwa barazani pa msemaji alikuwa:-

A. maiti
B. simba
C. farasi
D. sungura

**46.** Msemaji alilala fofofo kwa sababu:-

A. kuogopa askari
B. kuogopa mvua
C. kuogopa mnyama
D. alishikwa na wasiwasi

**47.** Ni nini ilimwambia kuna mnyama?

A. Mtu
B. Dhana zake
C. Mpita njia
D. Ndoto zake

**48.** Maiti iliyoonekana pale uani ilikuwa ya nini?

A. Simba
B. Askari
C. Msafiri
D. Mwizi

**49.** Kwa nini msemaji alifunga mlango kwa hofu?

A. Alioana simba
B. Aliona nyama kubwa
C. Aliona wezi
D. Aliona mwangaza

**50.** Kichwa kizuri cha habari hii ni:-

A. Ndoto usiku
B. Mnyama mkali
C. Msafiri
D. Usiku wa kutisha